

GOVERNMENT NOTICE No. 229

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO, 2014

- | | |
|----------------------------|--|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Eneo la matumizi Tafsiri | 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakavyoelekezwa vinginevyo;
"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo;
"Madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, kokoto, na mawe yanayochimbwa katika eneo la Halmashauri.
"Maeneo yasiyoidhinishwa" maana yake ni maeneo ya mito, madaraja, barabara, mashamba ya watu, mijini pamoja na maeneo mengine yanayofanana na hayo.
"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi. |

Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

Tangzao la Serikali Na. 229

“Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa na mnunuzi wa madini ya ujenzi.

“Wakala” maana yake ni mtu yejote, kikundi cha watu, kampuni, taasisi, asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Ukaguzi

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayekusudia kuanzisha machimbo katika eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba anatoa taarifa kwa Mkurugenzi ili eneo hilo likaguliwe kuhakikisha kwamba uchimbaji huo hautaenda kinyume na Sheria za Mazingira.

(2) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kukubali au kukataa eneo lolote kuwa au kutokuwa eneo la machimbo ya madini ya ujenzi.

Kibali cha uchimbaji

5.-(1) Mtu yejote anayetaka kuchimba madini katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuomba na kupata kibali cha kuchimba madini kutoka Halmashauri.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitaeleza aina ya madini yanayochimbwa na eneo litakalochimbwa madini hayo.

(3) Kibali kinachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitalipiwa ada ya shilingi elfu moja na mia tano tu (1,500/=)

(4) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga machimbo yoyote ya madini ya ujenzi kama itaona kufanya hivyo ni kwa maslahi ya umma.

Ushuru

6.-(1) Mtu yejote atakayesafirisha madini ya ujenzi kutoka eneo yalikochimbwa kwenda maeneo mengine atalipa ushuru kwa tripu kwa viwango vilivyooneshwaa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru huo utatozwa mara baada ya mnunuzi kununua madini kutoka kwa mchimbaji au kupakia madini hayo katika chombo ambacho atakitumia kwa ajili ya kusafirishia.

(3) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo, barabara zinazoelekeea au kutoka maeneo ya

machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

(4) Mnunuzi yejote atakayeshindwa kulipa ushuru anaotakiwa kulipa atatakiwa kupakua madini ya ujenzi kutoka katika chombo au kutochukua madini hayo mpaka hapo atakapolipa ushuru anaodaiwa.

Wajibu wa kulipa ushuru

7.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ushuru kulipa ushuru huo kama ilivyoelekezwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo kumzuia dereva au gari lolote kujishughulisha na usafirishaji wa madini ya ujenzi ikithibitika kwamba kuna ukiukwaji na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi.

Ushuru kulipwa kwa Halmashauri

8.-(1) Ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa kwa Halmashauri au wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha malipo hayo.

2 Itakuwa ni wajibu wa kila mtu aliyelipa ushuru kudai risiti na hautakuwa utetezi kwa mtu yejote kudai kuwa amelipa ushuru lakini hakupewa risiti.

Kufunika magari

9. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari au magari yanayobeba madini ya ujenzi kuhakikisha kwamba gari au magari yake yamefunikwa ili kuzuia uharibifu na uchafuzi wa Mazingira.

Muda wa machimbo kwa wazi

10. Maeneo yote ya machimbo ya madini yatafunguliwa kuanzia saa kumi mbili alfajiri na kufungwa saa kumi na mbili jioni.

Vituo vya ukaguzi

11.-(1) Halmashauri itaanzisha vituo kwa ajili ya ukaguzi wa magari yanayobeba madini ya ujenzi katika barabara zinazoingia na kutoka machimboni.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila dereva kusimama katika kituo cha ukaguzi wa madini na kuonyesha stakabadhi aliyolipa ushuru na endapo hatakuwa na stakabadhi hiyo atatakiwa kulipa ushuru kwa viwango vilivyoainishwa na

Sheria Ndogo hizi.

(3) Chombo chochote kitakachokamatwa kwenye eneo la machimbo na dereva au mmiliki wake akakimbia au kutoroka, hakitaruhusiwa kutoka mpaka dereva au mmiliki huyo atakapolipa faini ya shilingi elfu hamsini au muhusika kufikishwa mahakamani.

Halmashauri kutowajibika kwa hasara 12. Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mnunuzi au muuzaji wa madini ya ujenzi wakati wa kukusanya ushuru.

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa 13. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote yanapochimbwa madini ya ujenzi kwa ajili ya kukagua na kukusanya ushuru.

Kufifilisha kosa 14. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu ye yeyote iwapo mkosaji atakakiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyambatanishwa kwenye Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na kuwa tayari kulipa ushuru pamoja na faini anayodaiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi

Makosa 15. Mtu yeyote ambaye:

- (a) atakataa au kushindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Muidhiniwa;
- (b) atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
- (c) atakataa au kujaribu kukataa kulipa ushuru;
- (d) atashawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru;
- (e) atakwepa au atajaribu kukwepa kulipa ushuru;
- (f) atachimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyoidhinishwa;

Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

Tangza la Serikali Na. 229

- (g) atachimba shimo kubwa kwa ajili ya madini ya ujenzi na kuliacha bila kupanda miti au mimea mara baada ya madini hayo kuisha; na
- (h) atachimba madini katika eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri hasa maeneo ya barabara na maeneo ya hifadhi.

Adhabu

16. Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

(Chini ya Kifungu cha 7)

<i>Na</i>	<i>Aina ya madini ya Ujenzi</i>	<i>Ada ya kibali</i>
1	Mchanga	50,000/=
2	Kuvunja kokoto bila mashine	50,000/=
3	Kuchimba kokoto(kifusi)	500,000/=
4	Kuchimba marumaru	100,000/=
5	Kuchimba chokaa	100,000/=
6	Kuchimba udongo wa tofali za kuchoma	100,000/=
7	Mradi wa kutengeneza chokaa,marumaru	5 asilimia ya mauzo kwa mwaka

Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

Tangzao la Serikali Na. 229

JEDWALI LA PILI

<i>Na</i>	<i>Aina ya gari</i>	<i>Kiwango cha ushuru</i>
1	Gari lenye uzito wa kuanzia tani 1 na kuendelea	Asilimia 5 ya bei ya kununulia madini ya ujenzi.

JEDWALI LA PILI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi.....wa SLB..... ninaefanya biashara ya katika eneo la lililopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo. Nakiri kuwa leo tareheNilikiuka kifungu chacha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo za mwaka 2014. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeoyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliopewa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini

Mbele yangu..... (jina)

Saini

Wadhifa

Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

Tangzao la Serikali Na. 229

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 19 Mwezi Julai, 2013, na nembo ilibandikwa mbelea ya:-

IMELDA ISHUAZA,
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

MECKSON MOSES MWAKIPUNGA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

NAKUBALI,

Dodoma,
19 Mei, 2014

MHE. MIZENGO P. PINDA, (MB.)
Director General